



## ***Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo***

### **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11- 20 APRILI, 2023 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2023.**

#### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2023.**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilikua na mabadiliko kidogo wakati ile iliyopo katika kizio cha Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipunguwa nguvu. Hali hii iliuruhusu Ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo yaliyoko kaskazini mwa nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi lilikua la juu kidogo ya wastani hali iliyopelekea hewa yenye unyevunyevu kuvuma kutokea baharini kuelekea ukanda wa pwani. Joto la bahari la eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific lilikua la wastani. Joto la bahari la mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) lilikua la juu ya wastanina hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

#### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2023.**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria, magharibi, maeneo ya nyanda za juu kusini-magharibi na maeneo ya ukanda wa pwani. Maeneo ya kati na nyanda za juu kaskazini-mashariki yalipata mvua nyepesi hadi mvua za wastani.

### **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 21-30 APRILI, 2023.**

#### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21- 30 APRILI, 2023.**

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kizio cha Kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuwa na mabadiliko kidogo wakati ile iliyopo katika kizio cha

Kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kupunguwa nguvu. Hali hii iliuruhusu Ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusalia katika maeneo yaliyoko kaskazini mwa nchi yetu. Joto la bahari katika eneo la kusini- magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani, hali inayotarajiwa kuendelea kuruhusu upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea maeneo ya pwani ya nchi yetu. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pacific joto la bahari linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, hali hii itasaidia katika kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo nchini. Kwa upande mwingine, joto la bahari mashariki mwa bahari ya Atlantic (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 APRILI, 2023.**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Mvua zinazoambata na ngurumo za radi zinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua na ngurumo za radi zinatarajiwa kwa baadhi ya maeneo.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua na ngurumo za

radi kwa baadhi ya maeneo zinatarajiwa.

Imetolewa na;

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**